

## **Athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha**

**Joan Godwin Kileo**

**Tasinifu ya M. A. (Kiswahili)**

**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, 2017**

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza athari za Kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha. Utafiti huu una malengo mahususi matatu ambayo ni: kubainisha maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyomo katika lugha ya Kisiha, kueleza athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha, na kufafanua sababu za athari za kimofonolojia za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kisiha. Chanzo cha data kilichotumika katika utafiti huu ni uwandani. Data zilikusanywa kwa njia ya mahojiano, hojaji na ushuhudiaji kutoka kwa wazee wenye rika la kati ya miaka 50-85 na wanafunzi wa kati ya miaka 10-14 katika wilaya ya Siha. Data zilizopatikana katika utafiti huu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Makutano na Mwachano ya Giles (1982). Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa lugha ya Kisiha imeathiriwa na lugha ya Kiswahili hasa katika kipengele cha mofolojia. Aidha, athari za kifonolojia zimejitokeza katika kipengele cha sauti za Kiswahili zilizotumiwa na watoa taarifa wakati walipokuwa wanazungumza Kisiha. Athari hizo ni matumizi ya sauti [z] badala ya sauti [s], sauti [m] badala ya sauti [n], sauti [ch] badala ya sauti [sh] pamoja na udondoshaji wa sauti [h] ya Kisiha. Fauka ya hayo, utafiti huu umeweka bayana sababu za athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha, ambapo miongoni mwa sababu hizo ni elimu, biashara, pamoja na upanuzi wa matumizi ya Kiswahili vijijini. Mwisho ni muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti fuatishi ambapo imependekezwa kuwa tafiti zifanyike katika vipengele ambavyo havikushughulikiwa, kama vile sintaksia na semantiki. Aidha, kuna haja ya kufanya tafiti kuhusu mbinu na mikakati ya kuchochea matumizi ya lugha ya Kisiha katika muktadha huu wa kutamalaki kwa lugha ya Kiswahili ili kuweza kudumisha lugha ya Kisiha.